



OFISI YA WAZIRI MKUU

KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

MRADI WA KUKUZA AJIRA NA UJUZI – TANZANIA

(EMPLOYMENT AND SKILLS FOR EMPLOYMENT – TANZANIA (E4DT))

TAARIFA KWA UMMA

FURSA YA MAFUNZO YA UKUZAJI UJUZI KATIKA FANI ZA UCHOMELEAJI VYUMA VIWANDANI, UFUNDI BOMBA VIWANDANI NA UFUNDI BOMBA WA MAJUMBANI

1. **Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu** inashirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) kutekeleza mradi wa kukuza Ajira na Ujuzi kwa Maendeleo ya Afrika (E4D). Katika mwaka huu wa fedha Ofisi imepanga kutoa mafunzo ya ujuzi katika fani za Uchomeleaji vyuma viwandani (Industrial Welding), ufundi Bomba wa viwandani (Industrial plumbing) na ufundi Bomba wa majumbani (Domestic plumbing) kwa vijana 1,500 wenye umri kati miaka 15 hadi 35. Mafunzo haya yatatolewa na VETA kwa mfumo wa VSOMO (masomo ya ufundi stadi kwa njia ya mtandao/dijitali yakifuatiwa na mafunzo kwa vitendo vyuoni).
2. Mradi wa E4D unafadhiliwa na Wizara ya Shirikisho la Ujerumani ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (BMZ), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo wa Norway (Norad), Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Korea ya Kusini (KOICA).
3. Mafunzo yatafanyika kwa njia mbili ambazo ni: mafunzo ya VSOMO ya nadharia kwa njia ya mtandao kupitia simu janja au kishikwambi kwa muda usiozidi miezi miwili yakifuatiwa na mafunzo kwa vitendo vyuoni kwa wiki mbili. Baada ya mafunzo ya vitendo vyuoni,



Implemented by:



Jointly funded by:





wanafunzi watapata fursa ya kufanya mafunzo kwa vitendo viwandani chini ya uangalizi wa ATE na GOPA.

4. Vigezo vya kujiunga na mafunzo kwa njia ya VSOMO ni vifuatavyo:
 - a) Awe raia wa Tanzania.
 - b) Awe na umri kati ya miaka 15 hadi 35 (Idhini ya maandishi ya wazazi/walezi inahitajika kwa walio chini ya miaka 18 wakati wa mafunzo kwa vitendo viwandani.)
 - c) Aweze kuhudhuria mafunzo kwa vitendo katika moja ya vyuo vya VETA Dodoma, Lindi au Manyara katika muda wote wa mafunzo.
 - d) Awe na ujuzi au uzoefu wa miezi sita katika fani ya uhomeleaji na uungaji wa chuma, ufundi bomba wa viwandani au ufundi bomba wa majumbani.

5. Waombaji wanapaswa kupakua programu ya VSOMO kutoka **Playstore** katika simu zao au kwa watu walio karibu yao wenye vishikwambi au simu za android na kujiandikisha kwa kutumia programu ya VSOMO. Kwa maombi, hati/maelezo yafuatayo ni ya lazima kutoa:
 - a) Mzazi/mlezi awe tayari kugharamia mahitaji ambayo hayatafadhiliwa na mradi wakati wa kufanya mafunzo kwa vitendo vya vyuo.
 - b) Gharama za kuendesha mafunzo kwa VSOMO zitalipwa na mradi kwa ajili ya mwombaji ambaye atafanikiwa kumaliza mafunzo kwa njia ya mtandao na kufaulu kabla ya kuanza mafunzo ya vitendo katika vyuo tajwa.
 - c) Mfumo wa VSOMO kwa ajili ya kujiandikisha au kutuma maombi utafunguliwa tarehe 9 Novemba hadi 13 Novemba 2022.
 - d) Mwombaji atatakiwa kuingiza taarifa binafsi kwenye mfumo kama zilivyoainishwa. Mwombaji atatakiwa kuziwasilisha viambatanisho wakati wa kushiriki mafunzo ya vitendo chuoni.
 - i. Cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha Taifa au kadi ya mpiga kura au barua ya utambulisho kutoka Serikali ya Mtaa anakoishi mwombaji (lazima);
 - ii. Anwani ya makazi, nambari za simu na barua pepe (ikiwa inapatikana).

6. Vijana watakaofaulu mafunzo ya nadharia kwa njia ya VSOMO watagharamiwa na programu ya E4D kwa kulipiwa ada ya mafunzo kwa vitendo kwa wiki mbili.



Implemented by:



Jointly funded by:





7. Washiriki watakaochaguliwa watajulishwa kwa njia za barua pepe, SMS, tovuti za chuo husika cha VETA na Ofisi ya Waziri Mkuu (OWM-KVAU) kuanzia 14 – 19 Novemba, 2022. Mafunzo ya nadharia kwa njia ya mtandao yataanza rasmi 21 Novemba, 2022.

Kwa ajili ya kupata taarifa zaidi wasiliana na VETA KIPAWA ICT kwa barua pepe kictc@veta.go.tz au simu nambari +255 714 720 381 (Simu, SMS au WhatsApp).

Imetolewa na:

Katibu Mkuu,

Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana Ajira na
Wenye Ulemavu,

SLP 2890,

Dodoma.

ps@kazi.go.tz

Mkurugenzi Mkazi,

Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ),

SLP 1519,

Dar es Salaam.

giz-tanzania@giz.de



Implemented by:



Jointly funded by:

